JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

OLD SHINYANGA SEKONDARI

S.L.P 1218 – SHINYANGA.

Namba za simu: 30/3/2022

- Mkuu wa shule: 0769 020 723 / 0784 575 150
- Makamu Mkuu wa Shule; 0684 819 809 / 0756 696 879

Mzazi/Mlezi wa ……

S.L.P …….

……..……

YAH: <u>MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA - 2022</u>

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano chaguo la HKL/HGK/HGL/HGE/EGM – katika shule ya Sekondari Old Shinyanga iliyoko Mkoani Shinyanga. HONGERA SANA.

Unatakiwa kufika hapa shuleni ifikapo tarehe …..... . Utapokelewa na Makamu Mkuu wa Shule pamoja na mwalimu wa zamu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe …… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……na mwisho wa kuripoti ni tarehe …….

1. **USAFIRI:**

   Ufikapo mjini Shinyanga kama umeshukia kituo cha mabasi cha Shinyanga, panda pikipiki kwenda soko kuu ambapo utakuta hiace (mabasi madogo). Ziendazo Old Shinyanga kupitia shuleni na ushukie Old Shinyanga Sekondari karibu na kiwanda cha nyama

2. **MAHALI SHULE ILIPO:**

   Shule hii ipo kushoto kando kando ya barabara ya Old Shinyanga umbali wa kilometa 10 kutoka Shinyanga Mjini na imepakana na kiwanda cha nyama Old Shinyanga.

3. MAHITAJI:

(a) VIFAA

Vifaa vifuatavyo ni vya lazima mwanafunzi kuja navyo shuleni.

- Godoro (futi 2½ upana)
- Jembe jipya na mpini wake au fyekeo
- Ream 1 ya karatasi za photocopy (photocopy paper A4) kwa ajili ya mitihani yake ya kila wiki, mwezi na muhula. Hii itatolewa kila mwaka.
- Aje na soft broom/ufagio wa chelewa wa mpini kwa ajili ya usafi.
- Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya kuogea na kufulia
- Mto 1 na foronya za rangi ya pinki zisizo na maua
- Shuka 2 za kulalia rangi ya pinki au bluu bahari na chandarua
- Mahitaji yake binafsi mbalimbali
- Faili la kuhifadhi mitihani yake.
- Vyombo vya kulia chakula (kikombe, sahani, bakuli na kijiko)
- Blanket moja (la kawaida) **kwa wenye matatizo ya kiafya**.
- Daftari kubwa, counter book 8, kalamu za wino na penseli za kutosha.
- Scientific calculator (Casio Fx 991,) kwa michepuo ya EGM, HGL, HGE na HGK
- Aje na mathematical set.
- Aje na vitabu vya masomo ya tahasusi (Combination) yake.

NB: kutokana na umbali atokapo mwanafunzi, usumbufu wa kusafiri na mizigo mizito, anaweza kuja na kununulia baadhi ya mahitaji hapa shuleni mfano: (Daftari, counter books, mathematical set, kalamu, penseli, kandambili nk)

(b) SARE ZA SHULE (UNIFORM):

- Suruali mbili (2) za rangi ya kijani kwa ajili ya darasani na moja (1) nyeusi ya kushindia. Ashone mwenyewe. Ziwe na upana chini (18) na zisiwe za kubana.
- Sweta rangi ya kijani.
- Tai rangi ya kijani
- T- shirt yenye kola rangi kijivu nyeupe, inapatikana shuleni kwa Tsh.10,000/= Haruhusiwi kuja na mavazi ya nyumbani.
- Nguo za michezo anaweza aje na Track nyeusi au dark bluu, pia aje na raba za michezo.
- Aje na shati nyeupe (2) mikono mirefu.

- Aje na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye kisigino kifupi, jozi moja au Zaidi. Viatu visiwe vimechongoka mbele na viwe vya kamba.
- Soksi rangi nyeusi jozi 2
- Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

(c) ADA YA SHULE

- Ada kwa mwaka ni **Tshs.70, 000/=** au **35,000/=** kwa muhula, hakikisha unalipia ada hiyo benki **(NMB, AC/NO: 30701100046 – OLD SHINYANGA SEKONDARI)** na usije na pesa za ada mkononi. Pay in slip (Risiti ya malipo ya benki) **iwe na majina ya mwanafunzi na sio ya Mzazi/Mlezi.**

(d) MICHANGO MINGINE:

- Kitambulisho na picha Tshs. 6,000/=
- Matibabu Tshs. 10,000/= kila mwaka (Tshs. 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na Tshs. 5,000/= kwa ajili ya Bima ya afya). Kama mwanafunzi ana Bima ya afya atalipa Tshs. 5,000/= ya huduma ya kwanza.
- Ukarabati wa samani Tshs. 15,000/=
- Taaluma Tshs. 20,000/=
- Gharama za wapishi Tshs.30,000/=
- Mitihani ya kujipima (Mock) Tshs. 20,000/=
- Fedha ya tahadhari Tshs. 5,000/=
- Nembo ya shule Tshs.2,000/=
- Gharama za walinzi na vibarua wengine wa shule Tshs. 10,000/=

ANGALIZO: Jumla ya ada na michango kwa mwaka **Tshs. 188,000/=.**

Fedha yote ilipwe benki na mwanafunzi aripoti shuleni akiwa na **Bank pay in slip** yenye kuonyesha majina yake kamili.

NB: **Mwanafunzi ajapo shuleni anatakiwa kuja na Result slip ya kidato cha nne na nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)**

4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

- Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978. Unatakiwa kuzingatia (sheria) mambo ya msingi yafuatayo.

5. BAADHI YA SHERIA ZA MSINGI NI:

- Heshima kwa wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika shughuli zote za kila siku ndani na nje ya shule
- Kuzingatia kikamilifu mipaka ya shule na uwepo wa ndani ya mipaka hiyo wakati wote mwanafunzi akiwa shuleni.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- Kuvaa sare za shule wakati wote, mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi shuleni.
- Kuwahi katika shughuli zote za shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- Kutokuleta radio, simu ya mkononi au card au charger ya simu shuleni. Mwanafunzi akikutwa na kitu kimojawapo kati ya vitu hivyo adhabu yake ni kufukuzwa shule.
- Hairuhusiwi kutumia mshumaa au kibatari (kama ataweza awe na taa ya kuchaji au inayotumia betri au taa ya solar).

6. MWISHO

- Unaporipoti unatakiwa kukabidhi fomu ya ahadi ya mwanafunzi na ahadi ya mzazi/mlezi pamoja na fomu ya uchunguzi wa afya kwa Makamu Mkuu wa shule.

KARIBU SANA OLD SHINYANGA SEKONDARI

……..

MKUU WA SHULE

3. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa Ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule,

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(ix) Uvutaji wa sigara

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

(xii) Kusababisha mimba

(xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkonni katika mazingira ya shule.

(xv) Kudharau Bendera ya Taifa

(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

(xviii) Kutoroka/kulala nje ya shule bila ruhusa

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

Old Shinyanga Secondary School,

P. O. Box 1218,

SHINYANGA.

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

This form must be completed by a government medical officer.

Student's Full Name: ……...……...

Present age: …… Sex: ……..……

Blood test: ……Group:…….……..

Stool Examination: …….……

T. S. Test: ……...……...……..

Asthma: ……..……..

Eye disorder: …….……..

Nose disorder: ……..

Ear disorder: ……..……..

Skin disease: ……..

Anemia: ……..……..

Chest: …….……..

Operations: ……...……..

Serious accidents: ……..……

Any other infection disease: ……..……

Pregnancy …… (In case of female)

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical defects of impairments chronic of family disease etc.

……

……

I certify that I have personally examined Mr. /Miss ……..……

And found him/her/unfit to pursue further studies.

SIGNATURE: ……

DESIGNATION: ……

(Official rubber stamp)

STATION: ……

DATE: ……

SHULE YA SEKONDARI OLD SHINYANGA

FOMU YA KUKUBALI MWANAFUNZI

(ijazwe kwa **herufi kubwa** na **irejeshwe** kwa mkuu wa shule)

1. Jina kamili : …….....

   Tarehe ya kuzaliwa: …… Wilaya: …….. Mkoa: ……..

   Taifa: ……. Dini: ……..

2. Jina kamili la baba/mama/mlezi: ……..……..

   Anwani yake: ……..……

   Kazi ya baba/mama/mlezi: ……..……

   Namba ya simu: ……..……

AHADI YA MWANAFUNZI:

(a) Mimi ……nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Old Shinyanga kuanzia tarehe ……hadi nitakapomaliza kidato cha sita.

(b) Kwa hiyo naahidi kwamba;

(i) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.

(ii) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kama kushiriki migomo, fujo, makosa ya jinai n.k. najua pia SIMU, UTORO na UCHELEWAJI shuleni HAVIKUBALIKI.

(iii) Nitatunza mali za umma ambazo ni pamoja na majengo, samani, vitabu n.k.

Tarehe: …….. Sahihi ya mwanafunzi: …….

Sahihi ya Dole gumba

AHADI YA MZAZI/MLEZI:

Mimi: ……ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……. Naahidi kwamba;

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule, walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya Sekondari Old shinyanga. Iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongozi wa shule.
2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kusoma kwa kulipa ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule

   Sahihi: …….

   Tarehe: ……